**HOTUBA YA MHESHIMIWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN KWENYE HAFLA YA KUHITIMISHA MAADHIMISHO YA MIAKA 60 YA JESHI LA POLISI NA KUFUNGA MKUTANO MKUU WA MAAFISA WAANDAMIZI WA JESHI LA POLISI TAREHE 17 SEPTEMBA, 2024 MOSHI, KILIMANJARO**

- ***Mheshimiwa Mhandisi Hamad Masauni (Mb), Waziri wa Mambo ya Ndani ya nchi;***
- ***Waheshimiwa Mawaziri wote mliopo hapa;***
- ***Waheshimiwa Naibu Mawaziri;***
- ***Mheshimiwa Balozi Dkt. Moses Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi;***
- ***Mheshimiwa Eng. Zena Hamed Said, Katibu Mkuu Kiongozi Zanzibar;***
- ***Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu mliopo;***
- ***Mheshimiwa Nurdin Babu, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro;***
- ***Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb), Naibu Spika;***
- ***Mheshimiwa Vita Mfaume Kawawa (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya NUU;***
- ***Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya PAC;***

- ***Inspekta Jenerali wa Polisi, Camillus Mongoso Wambura, Mkuu wa Jeshi la Polisi;***
- ***Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama;***
- ***Ma-Inspecta Jenerali wa Polisi Wastaafu mliopo;***
- ***Makamishna wa Polisi;***
- ***Ndugu Sylivester Mwakitalu, Mkurugenzi Mkuu wa Mashtaka (DPP);***
- ***Mheshimiwa James Wilbert Kaji, Mkuu wa Wilaya ya Moshi Mjini;***
- ***Makamishna wa Polisi Wastaafu mliopo;***
- ***Viongozi Waandamizi kutoka Idara Mbalimbali za Serikali mliopo;***
- ***Maofisa Waandamizi wa Jeshi la Polisi mliopo;***
- ***Watumishi Raia mnaofanya kazi Jeshi la Polisi mliopo;***
- ***Viongozi wa Dini;***
- ***Wageni Waalikwa;***
- ***Wanahabari;***
- ***Mabibi na Mabwana.***

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Leo nina faraja ya kukutana nanyi hapa Chuoni Moshi, kwa kufanya mambo mawili makubwa. ***Kwanza,*** kuhitimisha maadhimisho ya miaka 60 ya Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. ***Pili,*** kufunga Mkutano Mkuu wa Maafisa Waaandamizi wa Jeshi la Polisi.

IGP hongereni sana, maadhimisho haya yamefana sana. Kilichonipa moyo sana ni kikosi cha watoto. Wanasema udongo upate ukiwa u maji. Sasa wale kuna wale watakaoenda kusoma sayansi na vitu vingine, lakini wale watakaobakia waingize ndani ya Jeshi, hapa ni kwao.

Mtakumbuka mara ya mwisho tulipokutana mwaka jana tarehe 4 Septemba, 2023, nilitoa maagizo kadhaa ambayo nilitaka Jeshi la Polisi liyafanyie kazi. La kwanza ilikuwa ni kushirikiana na TAMISEMI kuhakikisha tunaimarisha ulinzi katika jamii kupitia Polisi Kata. Nilisisitiza mabadiliko ndani ya Jeshi letu, na suala nililolisisitiza sio tu suala la kibajeti, hilo la bajeti ni la kwangu nimelifanyia kazi vizuri. Bali nilisisitiza mabadiliko ya kifikra na mitazamo (*mindset change*) kwa askari wetu wa Jeshi la Polisi. Suala la tatu Nililosisitiza ni umuhimu wa kukuza matumizi ya teknolojia na kuhakikisha

mifumo ya Jeshi la Polisi inasomana na mifumo mingine kama vile ya DPP na Mahakama.

IGP nakushukuru sana kwa kunialika katika kikao hiki, kwani hii ni fursa ya kutathmini utekelezaji wa mambo hayo yote niliyoyabainisha.

Nilikuwa naangalia, mara ya mwisho tulivyokutana nilimsema IGP kuhusu upandishaji vyeo, na yeye aliniambia angerudi kwangu. Ninashukuru ameweza kuwachuja na kupendekeza, na nami nimeweza kuwapandisha vyeo Naibu Makamishna 28, na Makamishna Wasaidizi Waandamizi 127 ambapo wengi wenu mpo hapa leo. **Ninawapongeza sana.**

Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kufungua mafunzo haya. Naamini mtazingatia mafunzo mliyopewa, lakini pia naamini utaratibu huu utakuwa endelevu, askari wanatakiwa wapate mafunzo kazini, ndani na nje ya nchi.

Ninafahamu pia, baada ya tukio hili, leo jioni mtakuwa na hafla ya kuwaaga wastaafu waliomaliza utumishi wao ndani ya Jeshi la Polisi. Kwa kuwa sitapata muda wa kuhudhuria hafla hiyo, nitumie fursa hii kuwapongeza wote ikiwemo wale ambao wametunukiwa nishani za miaka 60 ya Jeshi la Polisi, na ninawatakieni maisha mema.

***Mheshimiwa Waziri na Inspekta Jenerali;***

Nitumie fursa hii kuipongeza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Jeshi la Polisi kwa kazi kubwa inayoendelea kufanyika. Leo hii tunapojivunia ongezeko la watalii, ongezeko la uwekezaji wa ndani na kutoka nje ya nchi, na kuendelea kuimarika kwa uchumi wa nchi yetu, hayo yote yanakuja kwa sababu nchi yetu ni salama. Kwa hiyo tunaishukuru Jeshi la Polisi kwa mchango mkubwa wa kuiweka nchi yetu katika hali ya usalama.

Ninakumbuka, wakati ninashika dhamana hii mwaka 2021, nchi yetu ilikuwa inakabiliwa na wimbi la makundi ya kihalifu. Kutokana na hali hiyo, kote nchini kulikuwa na hitaji la kusogeza huduma za kipolisi karibu zaidi na wananchi. Kwa dhamira na utekelezaji mzuri, Jeshi limeweza kutembelea na kuona uwezekano wa kuweka huduma za kipolisi katika kila Kata ya Tanzania Bara na kila Shehia ya Tanzania Zanzibar. Katika kuimarisha usimamizi wa Polisi Kata, mnaendelea na kazi ya kuimarisha ofisi za Wakuu wa Polisi wa Mikoa (RPCs), na ninatambua kwamba Ofisi za RPCs katika mikoa 10 zimekamilika na Ofisi nyingine katika mikoa 9, kazi inaendelea. Tutaenda kuongeza bajeti ili RPC wote wawe na majengo ya kisasa na wafanye kazi kwenye majengo yenye hadhi na heshima ya ngazi zao. Jitihada hizi zimewezesha Jeshi la Polisi kuweza kwa kiasi kikubwa kupunguza uhalifu.

Pamoja na kwamba uhalifu haumaliziki na huibuka kwa misimu, ila ninalipongeza Jeshil a Polisi kwa kuweza kuimarisha ulinzi wa raia na mali zao.

Ninapotoa pongezi hizi, haimaanishi kwamba, kila kitu kiko vizuri, ***la hasha.*** Bado zipo changamoto katika utendaji wa Jeshi letu la Polisi, na ambazo Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuimarisha Taasisi za Haki Jinai imependekeza na kushauri Serikali na Jeshi la Polisi kuzifanyia kazi.

***Mheshimiwa Waziri na Inspekta Jenerali;***

Leo tunapoadhimisha miaka **60** ya Jeshi la Polisi la JMT, nitumie fursa hii kuzungumzia changamoto mojawapo tunayoendelea kukabiliana nayo, ambayo ni ajali za barabarani. Takwimu za Uhalifu na Matukio ya Usalama Barabarani, zilizochapishwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, inaonesha kuwa, kati ya mwaka 2022 na 2023 kumekuwa na ongezeko la vifo 100 vinavyotokana na ajali za barabarani. Mwaka 2022 ziliripotiwa ajali 1,720 zilizosababisha vifo **1,545** na mwaka 2023 zilitokea ajali 1,733 zilizogharimu maisha ya watu **1,645.** Kwa miaka hiyo miwili pekee, Tanzania ilipoteza watu **3,190**. Ni dhahiri kwamba, ajali za barabarani zinapaswa kutazamwa kwa jicho la karibu sana, tena kwa udharura.

Vyanzo vikubwa vitatu vya ajali za barabarani ni; sababu za kibinadamu (93.9%), ubovu wa vyombo vya usafiri (4.1%), na sababu za kimazingira ikiwemo ubovu wa miundombinu ya barabara (2.0%). Hii ni kusema kwamba

Serikali imefanya kazi kubwa kuboresha barabara, na Jeshi la Polisi limefanya kazi kubwa katika kukagua vyombo vya usafiri. Uzembe, ulevi na kutojali uendeshaji salama bado inachukua nafasi kubwa sana, sasa hili lipo ndani ya uwezo wenu, mnatakiwa kuendelea kulifanyia kazi, hususan kupitia elimu kwa raia. Tunaambiwa kwamba **asilimia 37.9** ya ajali zilizotokea mwaka 2023 zilitokana na uzembe wa madereva; **asilimia 21.2** mwendo kasi na **asilimia 13.6** uzembe wa madereva wa pikipiki. Vyote hivi vipo ndani ya uwezo wa Jeshi la Polisi, na mnaweza kuendelea kuchukua hatua kupunguza ajali barabarani.

***Ndugu IGP na Maofisa Waandamizi wa Jeshi la Polisi****;*

Nilipoanza hotuba yangu, nilizungumzia haja ya Jeshi la Polisi kubadilika kifikra na mitazamo. Nilipongeza hatua zinazochukuliwa za mafunzo ya kukuza ujuzi na maarifa yanayofanywa ndani na nje ya nchi. Jambo hili nataka niliunganishe na kauli mbiu ya Kikao Kazi hiki, isemayo ***'Huduma Bora za Kipolisi kwa Umma zitapatikana kwa kubadilika kifikra, Usimamizi wa Sheria na Matumizi ya TEHAMA'***. Ni Kauli Mbiu muafaka kwa mazingira tuliyonayo. **Kwanza,** ni kaulimbiu inayotambua kuwa kinachofanywa na Jeshi la Polisi ni huduma. **Pili,** kaulimbiu inaendeleza mabadiliko ya kifikra, ambao ni msingi mkuu katika kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai, ambapo suala la mabadiliko ya kifikra kwa Polisi limechukua nafasi kubwa. **Tatu,** pamoja na kuadhimisha miaka 60 tangu kuanzishwa kwake, Jeshi hili halitakiwi kuishi kihistoria, bali kuyaishi mazingira ya leo yanayoongozwa na matumizi ya

TEHAMA. Hapa nipongeze hatua iliyofikiwa na Jeshi la Polisi, nimepita kwenye banda la maonesho na kujionea matumizi ya teknolojia yalivyobadilika muda hadi muda ndani ya Jeshi la Polisi. Hivyo, jinsi dunia inavyobadilika, Jeshi letu nalo linatakiwa kubadilika kwa zana kulingana na mabadiliko hayo.

Hivyo basi, ninaamini katika Mkutano wenu huu, mlipata wasaa wa kuichambua Kauli mbiu hii, mmeona kipi mmeweza kutekeleza na kipi bado hakijatekelezwa na kwanini. Mtakaporudi kwenye vituo vyenu vya kazi uchambuzi huo utawaongoza katika utendaji wa majukumu mliyokasimiwa. Aidha, maadhimisho ya miaka 60 ya Jeshi la Polisi yawe fundisho kwetu sote kwamba, maendeleo ya dunia, yanafanya uhalifu nao ubadilishe mbinu, hivyo, upelelezi wake, na udhibiti wake ni lazima navyo vibadilike. Mabadiliko ya dunia tunayoyazungumzia ni ongezeko la matumizi ya mitandao na Akili bandia, ambayo ni lazima tuendelee kuiangalia kwa jicho la karibu. Tukiangalia suala la uhalifu wa njia ya mtandao unaotokana na ukuaji wa teknolojia, unatupeleka katika ulimwengu tofauti na tunaoujua au tuliouzoea. Katika eneo hili si lazima mtu kufanya uhalifu akiwa Tanzania, anaweza kuwa nje ya Tanzania na akafanya uhalifu nchini Tanzania. Ofisi ya Taifa ya Takwimu, ilichapisha taarifa inayoonesha Uhalifu wa Mitandaoni umeongezeka kwa asilimia 36.1 kutoka matukio **1006** mwaka 2022 hadi matukio **1,369** mwezi Disemba 2023.

Kwa mujibu wa Taarifa hiyo, miongoni mwa uhalifu unaoongezeka kwa kasi katika eneo hili ni kutoa taarifa za uzushi na uongo, kusambaza picha za ngono, matusi na unyanyasaji mitandaoni. Ni wazi kwamba, kutokana na maendeleo ya kiteknolojia, hususan teknolojia ya Akili Bandia, uhalifu wa kutoa taarifa za uzushi na uongo utaongezeka. Aidha, kuzidi kwa harakati za kisiasa kuelekea chaguzi za Serikali za Mitaa na uchaguzi Mkuu kunatarajiwa kuongeza uhalifu wa kutoleana kauli za kashfa, za kibaguzi na za uongo. Kwa hiyo, ni vizuri Jeshi la Polisi kujipanga vyema kiteknolojia dhidi ya uhalifu huu katika jamii yetu. Hatusemi, tufunge mitandao ya kijamii, au tuwafunge midomo wananchi kutoa maoni yao, lakini haijuzu kufumbia macho uhalifu kwa sababu eti unafanyika mtandaoni. Uhalifu ni uhalifu, kama ambavyo mhalifu angekamatwa na kushtakiwa kwa kutoa kauli ya uchochezi nje ya mtandao wa kijamii, hatua hizo pia zichukuliwe akifanya uhalifu huo kwenye mitandao wa kijamii. Ni muhimu pia kuwa na uwezo na ujuzi wa kubaini wahalifu wanaojificha kwa kutumia majina bandia au kwa kutumia anga la nje ya Tanzania.

***Mheshimiwa Waziri na Ndugu IGP****;*

Suala jingine kwenye mitandao ni utapeli wa fedha ambao nao unafaa kuangaziwa kwa karibu. Ongezeko la utapeli wa kifedha mtandaoni na utoroshaji wa fedha kwa kutumia mitandao. Kama mnavyofahamu, Serikali inafanya jitihada kubwa za kujenga uchumi wa kidijitali kwa kurahisisha huduma

za kifedha kwa njia ya mtandao ili kuharakisha shughuli za uzalishaji mali na biashara. Kadri wananchi na wafanyabishara wanavyohamasika kufanya miamala kielektroniki, ndivyo wahalifu nao wanavyojaribu kubuni mbinu za kufanya uhalifu. Kwa mfano, kati ya Januari hadi Disemba, 2023 wananchi mbalimbali walitapeliwa jumla ya **shilingi bilioni 5 (5,067,205,056)** na Jeshi la Polisi, kwa vifaa na uwezo mdogo walio nao, waliweza kuokoa **shilingi milioni 288 (288,725,050)** ya kiasi kilichoibwa.

Kwa kuwa mwelekeo wa Serikali ni kupunguza matumizi ya fedha taslimu na kuongeza matumizi ya huduma za fedha kidijitali, ni lazima Jeshi la Polisi liwe na mkakati wa kupambana na uhalifu huu. Tunapoadhimisha miaka 60 ya Jeshi la Polisi, lisionekane kuzeeka, bali lionesha kupevuka na kuimarika. Nalitaka Jeshi la Polisi pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, liniletee mkakati wa kupambana na utapeli mitandaoni, ili tuone tunachoweza kufanya kuliwezesha Jeshi letu kuweza kupambana na uhalifu huu.

Jambo jingine ninalotaka kuzungumza nanyi ni kuhusu maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika tarehe 27 mwezi Novemba mwaka huu na Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwakani. Katika kipindi cha uchaguzi kila mmoja wetu anatakiwa kujipanga kufanya kazi zake vizuri zaidi. Tumejipambanua kulileta Taifa pamoja, hivyo, ni jukumu la kila mmoja wetu kuhakikisha Taifa letu linabaki kuwa moja na salama. *Uchaguzi utapita lakini*

*Tanzania itabaki!.* Tunataka kubaki na Tanzania iliyo salama na Tanzania yenye tulivu, ili shughuli za maendeleo ziweze kuendelea. Hivyo, ninalitaka Jeshi la Polisi kuwa macho katika kipindi chote cha kabla, wakati na baada ya uchaguzi. Polisi ihakikishe yeyote anayejaribu kuhatarisha amani ya nchi yetu kwa kisingizio cha chaguzi hizo, anachukuliwa hatua haraka na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria.

Inahuzunisha kuwa nchini kwetu kumekuwa na matukio ya kujirudia ya ukatili na mauaji ya watu wanaoishi na ualbino na watu wengine yanayohusishwa na upigaji ramli na vuguvugu la uchaguzi, matukio mengine ya mauaji yanahusishwa na imani za kishirikina katika uchimbaji madini. Tumeshuhudia mauaji ya watu wazima na watoto kwa imani za kishirikina, kama ulivyoibuliwa na Jeshi la Polisi hivi karibuni. Kumekuwa na matukio ya wapenzi kuuwana, wazazi kuua watoto wao au watoto kuuwa wazazi wao kikatili kabisa, na kisha kuchoma maiti moto, wengine wanakatwa vipande vipande na kufukiwa, na mambo ya aina hiyo. Huku ni kuondokwa na utu na ni uhalifu mkubwa sana. Wananchi wanakata tamaa kuona matukio haya yanahusisha sio tu waganga wa kienyeji, bali hata watu mashuhuri kama viongozi wadini na hata wazazi wa watoto. Inasikitisha kuona kuwa mambo haya ya mauaji yanatokea katika maeneo tunayoishi, inawezekana wananchi tunayaona lakini hatutoi taarifa. Ni mpaka mauaji hayo yaibuliwe na vyombo vya ulinzi, ndipo wengine tunakuwa na midomo kuchangia, kulaumu na kulaani.

Siku kadhaa zilizopita nchi yetu imepata msiba kwa kuuwawa kwa mmoja wa viongozi wa chama cha Siasa CHADEMA, kifo kilichosisimua miili na akili za sisi wananchi wa Tanzania, na kuibua hisia kali hususan kwa wafuasi wa CHADEMA. Katika hali ya kushangaza kifo hicho kimeleta hisia kali pia kwa wawakilishi wa baadhi ya mataifa ya nje wanaowakilisha nchi zao hapa kwetu. Nataka niungane nao na niseme kwa sababu yoyote ile, mauaji haya hayakubaliki, na ndio maana Serikali tuliyalaani na kutaka uchunguzi wa haraka ufanyike. Ndivyo inavyofanyika duniani kote.

Ndugu zangu Watanzania, maisha ya mwanadamu yeyote yule yana thamani isiyomithilika. Huwezi kufananisha uhai wa mwanadamu kwa ubora kwa hadhi, kabila, asili na jinsia, umri, au umajumui wake. Katika hali yoyote ile uhai wa mwanadamu ni jambo adhimu sana, na ndio maana uhai wa Mtanzania unalindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 14 ambayo inasema ***'Kila mtu anayo Haki ya Kuishi na kupata kutoka katika jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa Sheria'***. Kwa wote tunaotumikia wananchi katika nyadhifa mbalimbali Serikalini huwa tunapitishana kwenye kiapo cha kulinda katiba ya nchi katika kutimiza majukumu yetu. Sasa, nimtake kila mmoja wetu awajibike kwa kiapo alichoapa.

Baada ya tukio lile nimekuwa nikifuatilia maoni ya viongozi wa vyama vya siasa, viongozi wa dini, baadhi yao wakiniomba nikemee mambo hayo. Maoni

ya wazee mashuhuri (Butiku), wawakilishi wa mataifa ya nje hapa nchini, Jumuiya za Kiraia na wananchi kwa ujumla. Hisia za makundi yote niliyoyataja zikiibuliwa na kifo kimoja cha ndugu yetu Kibao. Makundi yote hayakukemea vifo vya kikatili vilivyokuwa vikitolewa taarifa kwa nyakati tofauti.

Nimesikiliza kwa makini maelezo yaliyotolewa na Katibu Mkuu wa CCM, *Clip* ya Mheshimiwa Slaa wa CHADEMA na vilevile *clip* ya Ndugu **Joseph Yona** wa Chalinze wote wakitoa taswira ya mipango ya uvunjifu wa amani inayopangwa na kutekelezwa na baadhi vyama vya siasa. Nayaunganisha haya na maamuzi ya kikao cha tarehe 11 Septemba, 2024 kilichofanywa na chama kimoja cha siasa kule Ngulelo, Mkoani Arusha. Kikao ambacho kimeazimia kuwatumia na kuwachochea vijana kwa kuzusha tuhuma dhidi ya Jeshi la Polisi, kufanya siasa chonganishi kwenye misiba, na kushusha morali kwa Jeshi la Polisi ili washindwe kufanya kazi yao ya kulinda usalama wa raia na mali zao.Nawashukuru kwamba katika kikao kile kilibani na kilitambua kwamba nchi hii ina inteligensia kubwa sana na walipeana onyo kwamba wajitahidi kuendesha mipango yao hasi kwa kutumia uhuru waliopewa na falsafa ya 4R.

Sasa kwa kutumia kofia ya Amiri Jeshi Mkuu katika nchi hii, niseme kwamba tumeapa kuilinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na kwamba tutafanya kila linalowezekana kuimarisha ulinzi wa maisha na uhai wa Watanzania kwa kuwa ni jukumu letu. Kwenye wajibu huu

wala hatuhitaji kuelekezwa na mtu yeyote nini cha kufanya, kwa sababu Katiba yetu inatupa maelekezo ya jinsi ya kuendesha nchi yetu. Hakuna mtu anayeumia na vifo hivi zaidi yetu sisi Watanzania, inayomwagika ni damu yetu. Wengine wakitaka kuonesha huruma yao basi tunawanasihi wafanye hivyo kwa kufuata makubaliano ya mahusiano ya Kidiplomasia ya Kimataifa kama ilivyoelezwa vyema kwenye *Vienna Convention on Diplomatic Relations*, ya mwaka 1961. Ni imani yangu kwamba tamko lililotolewa si maekelezo ya Wakuu wa Nchi wa kule walikotoka. *Hatuko hapa kuelekezwa nini cha kufanya ndani ya nchi yetu!*

Serikali yetu inaongozwa na falsafa ya Maridhiano, Kustahamiliana, Kubadilika na Kujenga upya Taifa letu. Falsafa hii ilikuja baada ya kuona Taifa limegawanyika kutokana na tofauti zetu kisiasa na kiitikadi. Falsafa hii ilikuja ili watu tutangulize Utaifa na Utanzania kwanza kabla mengine yoyote. Kama nchi na Taifa tumefarijika kuona kwamba Falsafa hii kwa kiasi kikubwa imeweza kuliunganisha Taifa letu. Hata hivyo, tunapotekeleza Falsafa ya R4 sio kuwa tumetupilia mbali sheria za nchi au tumeruhusu utovu wa nidhamu nchini, ***la hasha*;** sheria zipo, mila zipo, miongozo iko palepale. Hivyo basi, baada ya kazi hii nzuri ya kuliunganisha Taifa kupitia R4, hatutavumilia vitendo vyovyote vya kuleta machafuko na mifarakano nchini.

Ni vizuri tusisahau mapema mapito yetu, na juhudi zilizofanyika kutufikisha tulipo. Serikali imejitahidi sana kurejesha uhuru wa vyama vya siasa; uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa raia kwa ujumla. Wale waliokuwa uhamishoni walirejea nchini, wale waliokuwa na kesi za jinai tulizifumbia macho, na wengine waliokuwa jela waliotolewa, sasa wako huru na wanaendelea na shughuli zao ikiwemo shughuli za kisiasa. Lengo letu likiwa kuwaleta watu pamoja ili tuweze kujenga nchi yetu. Sasa watu walewale wameposahau yote hayo, na wanapofanya vitendo na kutoa kauli zinazojaribu kuturudisha nyuma, sisi hatutakuwa tayari kuwaruhusu kufanya hivyo. Amani na utulivu wa nchi yetu tutailinda kwa gharama yeyote ile. Niliwahi kusema na hapa nirudie tena kwa msisitizo, ***ukimya wangu sio ujinga, na wala kuongea sana kwa wale wanaongea sana sio werevu***. Anayekaa kimya sio mjinga, ni mtu anayetafakari mambo. Mliponikabidhi dhamana hii, niliapa kulinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na dhamana yangu pamoja na vyombo vya ulinzi ni kulinda amani ya nchi yetu, hivyo sitakuwa na muhali kwa yeyote anayetaka kuvuruga amani ya nchi yetu. Tumevumiliana kwenye mengi, lakini kwenye kulinda tunu ya amani na utulivu wa nchi, nirudie, **sitakuwa na muhali** kwa yeyote anayejihusisha na mambo hayo: anayeratibu, anayeshiriki na anayetekeleza mipango hiyo miovu.

***Mheshimiwa Waziri, Ndugu IGP na Maofisa Waandamizi wa Jeshi la Polisi****;*

Kabla sijahitimisha hotuba yangu, nina maelekezo yafuatayo.

***Kwanza,*** Wizara na Jeshi la Polisi muendelee kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuimarisha Taasisi za Haki Jinai kwa ukamilifu, muendelee kutekeleza mapendekezo yote yasiyohitaji mabadiliko ya Sheria au ongezeko kubwa la bajeti;

***Pili,*** kama walinzi wa raia na mali zao, Jeshi la Polisi ndio wasimamizi wa haki na Sheria. Hivyo, halipaswi kuhusishwa au kuhisiwa kuhusika na ukiukwaji wa Sheria na haki inazosimamia. Hivyo, endeleeni kusimamia kwa karibu maadili ya askari ili, Jeshi litoe huduma stahiki na kuongeza imani ya wananchi kwa chombo chao hiki;

***Tatu,*** Jeshi la Polisi linafanya kazi katika zama za kidijiti, hivyo kasi yake ya kuikumbatia TEHAMA inatakiwa kuwa kubwa zaidi. Kufanya hivyo sio tu tutaimarisha utendaji kazi, zaidi tunafanya hivyo ili Jeshi liweze kudhibiti uhalifu na wahalifu kwa ufanisi zaidi. Kwa hiyo, kamilisheni taratibu ili miradi ya Miji Salama (*Safer cities*), Ukaguzi wa Magari wa Lazima (*Mandatory Vehicle Inspection*) na Mradi wa *High way Road Patrol* ianze kutekelezwa. Katika kutekeleza miradi hiyo, hakikisheni Askari wanajengewa uwezo stahiki.

Sambamba na hayo, niitake Wizara kusimamia utekelezaji wa maelekezo ya Serikali kuhakikisha mifumo inasomana, ikiwemo mifumo ya Polisi na Mahakama na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali.

Nihitimishe kwa kuwashukuru tena kwa kunialika kwenye tukio hili lililofana. Ninawapongeza sana kwa maandalizi mazuri, na kwa kuona umuhimu wa kuadhimisha miaka **60** ya Jeshi la Polisi. Wataalam wanasema ili uweze kujua kama unafanikiwa ni vizuri kutazama ulikotoka. Tumepita kwenye maonesho tumeona hatua kubwa iliyopigwa; na hata kwenye miaka hii mitatu kuna hatua kubwa sana ambayo imepigwa. Niwapongeze, yapo mengi ya kujivunia, na yapo ya kuboresha kama ilivyobainisha na Tume ya Haki Jinai.

Ahadi yangu kama Amiri Jeshi Mkuu na Mkuu wa Nchi, ni kuendelea kuimarisha huduma za Polisi, ili pamoja na kuhakikisha usalama wa raia na mali zao, huduma hizo pia zisaidie kuchochea ukuaji wa uchumi wetu na ustawi wa jamii kwa ujumla. Ni matumaini yangu kuwa, mliyokubaliana kwenye Mkutano wenu, na maelekezo na mwelekeo tulioutoa leo, mtaviingiza kwenye programu zenu za utekelezaji ili mkutano ujao tuweze kupimana vizuri kwenye utekelezaji.

Baada ya kusema hayo, sasa natamka kuwa, *“Maadhimisho ya Miaka 60 ya Jeshi la Polisi na Mkutano Mkuu wa Mwaka 2024 wa Maafisa Wakuu Waandamizi wa Jeshi la Polisi yamefungwa rasmi”.*

Ahsanteni kwa kunisikiliza.